- Inaongeza hatari ya uchafuzi wa kemikali kwenye bidhaa pale miti isiyoruhusiwa itatumika
- Inahitaji nguvu kazi kubwa kukamilisha uchakataji
- Inahitaji muda wa kutosha kukamilisha uchakataji

## Kukaanga samaki

Njia ya kuchakata samaki kwa kutumia mafuta ya kula kwa kukaangia ili kuondoa maji na kuondoa vimelea na kuvifanya visilete uharibifu wa samaki.

### *Faida ya Kukaanga*

- Inaongeza radha ya aina ya bidhaa
- Inahitaji eneo dogo la kufanya uchakataji
- Haitegemei hali ya hewa kuwezesha uchakataji
- Inaongeza muonekano na rangi ya kuvutia katika bidhaa
- Inaongeza muda wa kuhifadhi na utunzaji wa bidhaa
- Gharama ya upatikanaji wa nishati ni ndogo
- Inahitaji muda mfupi kukamilisha uchakataji

### *Hasara za kukaanga*

- Inahamasisha ukataji wa miti na kupunguza uoto wa asili
- Inahitaji muda wa kutosha kukamilisha uchakataji

## *Kugandisha* na *Kupoza*

### *Faida ya Kugandisha na Kupoza*

- Inahitaji eneo dogo la kufanya uchakataji
- Haitegemei hali ya hewa kuwezesha uchakataji
- Inaongeza muda wa kuhifadhi na utunzaji wa bidhaa
- Inahitaji muda mfupi kukamilisha uchakataji
- Inalinda uasili wa bidhaa
- Unaweza kusafirishwa umbali mrefu

### *Hasara za Kugandisha* na *Kupoza*

- Gharama kubwa za kugandishia na kuhifadhi
- Inahitaji uangalizi mkubwa

### *Kuchemsha kwa mvuke*

Njia hii sana sana inatumika kuchakata ngozi za samaki kwa ajili ya kutengeneza unga wa samaki kwa matumizi ya mifugo

### *Faida zake*

- Inaongeza muda wa kuhifadhi na utunzaji wa bidhaa
- Inahitaji eneo dogo la kufanya uchakataji
- Haitegemei hali ya hewa kuwezesha uchakataji

### *Hasara zake*

Gharama kubwa ya kupata nishati.


Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

**AFISA MFAWIDHI WA KANDA**

**NA MSIMAMIZI WA MRADI (TASP II)**

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI

NA VIWANGO KANDA YA ZIWA VICTORIA

S.L.P. 1213 MWANZA

**SIMU**

+255 28 2550864

+255 754/784 437234

**Barua Pepe:** nfqcl_mz@yahoo.co.uk

**Tovuti:** www.nfqcl.go.tz


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

**IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI NA VIWANGO**



# Utayarishaji na Uhifadhi wa Mazao ya Uvuvi

**TRADE AND AGRICULTURE SUPPORT PROGRAMME II (TASP II)**


*Imetayarishwa na Maabara ya Kitaifa ya Samaki chini ya Mpango wa TASP II kwa ufadhili wa mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (EDF)*

## Utangulizi

Hii inahusisha mchakato mzima kuanzia pale samaki anapovuliwa katika maji hadi kumfikia mlaji akiwa katika ubora na usalama unaostahiki kwa ajili ya kulinda afya ya mlaji.

### Madhumuni ya Uchakataji

- Kupunguza kasi ya kuharibika na kuzuia upotevu wa viasili
- Kulinda usalama na afya ya mlaji
- Kurefusha kipindi cha kutumika na utunzaji wa mazao yaliyochakatwa
- Kuongeza thamani ya zao
- Kuzalisha bidhaa mbalimbali kulingana na matakwa ya mlaji
- Kurahisisha uhifadhi na usambazaji
- Kuboresha radha ya aina ya bidhaa

### Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uchakataji

- Eneo maalum linalokusudiwa kwa ajili ya uchakataji
- Vifaa/malighafi kwa ajili ya kazi husika
- Hali ya afya na usafi wa wahudumiaji
- Upatikanaji wa maji safi na salama
- Kuweka mfumo wa udhibiti wa taka ngumu na maji taka
- Eneo la kuhifadhia malighafi na bidhaa
- Upatikanaji wa aina ya vifungashio
- Pawepo na uzio kudhibiti wanaoingia na kutoka katika eneo la uchakataji

### Aina za Uchakataji

- Kukausha kwa jua
- Kukausha kwa chumvi
- Kukausha kwa moshi
- Kukaanga
- Kugandisha
- Kupoza
- Kuchemsha kwa mvuke

## Kukausha kwa Jua

Njia ya kuchakata samaki kwa kutumia nishati ya jua ili kuondoa maji na kuondoa vimelea na kuvifanya visilete uharibifu wa samaki.

### Faida za kukausha kwa jua

- Gharama ya nishati ni rahisi
- Kupunguza gharama za ujazo
- Aina ya wateja ulionao na soko
- Kurahisisha ubebaji na ufungashaji
- Gharama ya vifaa vinavyohitajika si vya gharama kubwa

### Hasara ya kukausha kwa jua

- Haitumiki wakati wa kipindi cha mvua au mawingu
- Inahitaji eneo kubwa la uchakataji
- Unahitaji muda mrefu kukamilisha uchakataji
- Unahitaji idadi kubwa ya watendaji
- Kuongeza gharama ya kuandaa vichanja

## Kukausha kwa Chumvi

Njia ya kuchakata samaki kwa kutumia madini ya chumvi ili kuondoa maji na kuondoa vimelea na kuvifanya visilete uharibifu wa samaki.

### Faida za kukausha kwa Chumvi

- Eneo dogo uhitajika kwa ajili ya uchakataji
- Gharama ya kuthibiti muingiliano ndani ya eneo la uchakataji ni ndogo
- Inaongeza radha na madini katika aina ya zao
- Haitegemei sana hali ya hewa
- Inapunguza kasi ya ukuaji wa vimelea




### Hasara ya kukausha kwa chumvi

- Inaongeza vimelea wanaopenda chumvi
- Inapunguza wateja hasa wanaojiami magonjwa yatokanayo na chumvi
- Inaongeza gharama ya upatikanaji wa chumvi
- Inaweza kuongeza uchafuzi wa kikemikali katika bidhaa husika

## Kukausha kwa moshi

Njia ya kuchakata samaki kwa kutumia moshi ili kuondoa maji na kuondoa vimelea na kuvifanya visilete uharibifu wa samaki.

### Faida ya kukausha kwa moshi

- Inaongeza reha ya aina ya bidhaa
- Inahitaji eneo dogo la kufanya uchakataji
- Haitegemei hali ya hewa kuwezesha uchakataji
- Inaongeza muonekano na rangi ya kuvutia katika bidhaa
- Inaongeza muda wa kuhifadhi na utunzaji wa bidhaa

### Hasara za ukaushaji wa moshi

- Inahamasisha ukataji wa miti na kupunguza uoto wa asili